

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

SHULE YA SEKONDARI MWAKIJEMBE,

S.L.P 2025,

TANGA.

MWANAFUNZI.....

S.L.P 6005.

TANGA.

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWAKIJEMBE KIDATO  
CHA KWANZA 2021.**

**1.0.** Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Mwakijembe. Shule ipo Wilaya ya Mkinga, Tarafa ya Mkinga, Kata ya Mwakijembe. Umbali wa Km 28 kutoka barabara kuu itokayo Tanga mjini kwenda Horohoro.

**2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.1 Sare ya shule

**(a) Wasichana**

- Sketi mbili (2)ndefu za rangi ya damu ya mzee.
- Mashati mawili (2)meupe mikono mifupi na juba jeupe kwa wasichana watakaopenda kuvaa hijabu.
- Viatu vyeusi vya kamba jozi mbili (2).
- Soksi nyeupe.

**(b) Wavulana**

- Suluari mbili (2)za rangi ya damu ya mzee.
- Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi.
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba jozi mbili (2).
- Soksi nyeupe
- Mkanda rangi nyeusi.

***Upana wa suluari chini – 14 inch***

(c) Nguo za michezo Track nyeusi kwa wasichana na Bukta nyeusi kwa wavulanana T-shirt nyekundu kwa wote.

(d) Madaftari 12, mkebe wa hesabu na Dictionary.

(e) T-shirt ya shule -Tsh.10,000 zinapatiakana shuleni.

.....  
CHABAYANGA S.Y  
MKUU WA SHULE

**KIAMBATANISHO “A”**  
**SHERIA ZA SHULE**

01	<b>HESHIMA</b>	Wanafunzi wanatakiwa kuwa na <b>HESHIMA</b> wa kiwandani au nje ya shule.
02	<b>MAHUDHURIO</b>	Mahudhurio shuleni na darasani ni muhimu kwa mwanafunzi.
03	<b>KUWAHI</b>	Wanafunzi wanatakiwa kuwahi na kuepuka kuchelewa kusikokuwa na sababu za msingi.
04	<b>SARE ZA SHULE</b>	Wanafunzi wanatakiwa kuwa na sare nzuri, safi naya heshima na kuivaa wakati wote anapotakiwa kufanya hivyo.
05	<b>MIPAKA YA SHULE</b>	Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo, mapumziko au wakifanya shughuli zingine isipokua kwa kibali maalumu. Pia hawatakiwi kutembelea vilabu vya pombe, majumba ya starehe, majumba ya kufikia wageni, nk.
06	<b>USAFI</b>	Wanafunzi wanatakiwa kuzingatia usafi wa mwili, mavazi na mazingira.
07	<b>NYWELE</b>	Mwanafunzi atakapofika shuleni awe amekata nywele robo nchi na zisiwe zimewekwa dawa. Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele.
08	<b>NGUO</b>	Nguo za nyumbani haziruhusiwi.

**3.0: MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE:**

- (a) Wizi.
- (b) Uasherati, Ubakajina Ushoga.
- (c) Ulevi na matumizi ya Madawa ya kulevya.
- (d) MakosayaJinai.
- (e) Kupiga au Kupigana.
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
- (g) Kudharau Bendera yaTaifa, picha zaViongozi wa serikali, Nembo yaTaifa, Wimbo wa Taifa na Fedha za Taifa.
- (h) Kuoja au Kuolewa.
- (i) Kupata mimba au kusababisha kupata mimba ndani na nje ya shule.
- (j) Kutoa au kusababisha kutoa Mimba.
- (k) Kugoma, Kuchochea/ Kuongo za mgomo au kuvuruga amani na usalama wa watu.
- (l) Kukataa Adhabu kwa makusudi.
- (m) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
- (n) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkomoni.

Ninatamka kwamba nimezisoma sheria hizi na ninaahidi kuzitekeleza kikamilifu, wakati wote.

**SAINI YA MWANAFUNZI.....**

**TAREHE.....**

**JINA LA MZAZI/ MLEZI .....**

**SAINI YA MZAZI/ MLEZI .....**

**TAREHE .....**

**KIAMBATISHI “B”**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI ULIOPEWA**

**SEHEMU A: TAARIFA ZA MWANAFUNZI (*Ijazwe na mwanafunzi*)**

1. Jinakamili:..... (*maji na matatu*)
2. Shule atokayo:.....
3. Tarehe ya kuzaliwa:..... Dini .....
4. Namba ya cheti cha kuzaliwa: .....
5. Mahali unapoishi sasa hivi:.....
6. Anuani .....

Mimi ..... ambaye maelezo yangu ni hayo hapo juu,  
nimesoma maagizo yote ya kujiunga na shule ya sekondari Mwakijembe na ninakubali kutimiza masharti  
yote, yaliyoagizwa na kutii sheria za shule. Ninaahidi kwamba niwapo shuleni nitazingatia maelekezo  
yote yanayotolewa mara kwa mara na walezi wangu ilikupata taaluma bora na maadili yanayotakiwa.

Saini yamwanafunzi .....

Tarehe .....

**SEHEMU B: TAARIFA ZA MZAZI/ MLEZI (*Ijazwe na mzazi/ mlezi*)**

1. Jinakamili :.....
2. Namba ya NIDA: .....
3. Kazi:.....
4. Mahali unapoishi: .....
5. Anuani/namba ya simu:.....
6. Saini ya mzazi/mlezi: .....
7. Tarehe .....